# HOTUBA YA MWENYEKITI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA MHE. NYAULINGO A. BULAMLETE

## KATIKA KIKAO CHA KUVUNJA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 08.07.2015

***Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri,***

***Mhe.Mkuu wa wilaya,***

***Wahe. Wabunge,***

***Wahe. Madiwani,***

***Mkurugenzi Mtendaji,***

***Wakuu wa Idara na Vitengo,***

***Watumishi wote wa Halmashauri,***

***Viongozi wa siasa,***

***Viongozi wa Madhehebu ya Dini,***

***Wageni waalikwa,***

***Wananchi wote kwa ujumla,***

***Mabibi na Mabwana!.***

Awali ya yote sina budi kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima huu tulionao.

Lakini niwashukuru ninyi nyote kwa kuhudhuria mkutano huu wa kuvunja baraza la Madiwani na kuagana.

Katika kipindi chote cha miaka mitano, tulishirikiana kwa pamoja, leo hii tunavunja Baraza la Madiwani na kuagana .Katika kipindi chote cha miaka mitano tuliishi kama ndugu na tuliweza kutekeleza majukumu yetu sisi kama wawakilishi wa wananchi na watendaji. Huduma zimezidi kuimarika lakini miradi mingi ya maendeleo imetekelezwa na inaonekana kupitia Sekta ya Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Afya, Maji, Elimu, Kilimo, Ujenzi na Biashara.

Ni furaha pia kwakuwa tumeshirikiana vizuri na kujenga timu imara katika kuwaletea wananchi wetu maendeleo endelevu.

Kutokana na mazoea ya ushirikiano katika utendaji wetu tuna achana kwa muda huku tukiwa na kumbukumbu nzuri ya ushirikiano mzuri, tulishibana na kusaidiana sana katika harakati za kulijenga taifa hili kupitia uwakilishi wetu katika Baraza la Halmashari ya Wilaya ya Mpwapwa. Hata hivyo ni imani yangu kwamba huzuni hii haitadumu kutokana na kazi kubwa tuliyoifanya katika kipindi hiki cha miaka miaka 5 (2010 – 2015) na hivyo kurahisisha maamuzi ya wananchi ya kutupatia ridhaa ya kuwatumikia kwa awamu nyingine kwa lengo la kuongeza kasi ya kuwaletea Maendeleo Wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa. Tuombeane Heri na

kwakuwa Mwenyezi Mungu ni Mwaminifu tutaungana tena baadae mwaka huu ( Novemba 2015).

Kwa namna ya pekee kabisa ninakushukuru Mkurugenzi mtendaji pamoja na timu ya wataalamu kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya kwanza kwa kushirikiana nasi vema lakini pia kutekeleza maazimio mbali mbali ambayo tuliyapitisha kwa ajili ya ujenzi wa ustawi wa jamii yetu na taifa kwa ujumla. Mmekuwa mkifanya kazi bega kwa bega, usiku na mchana, kwa uzalendo mkubwa tangu safari ya baraza hili ilipokuwa imeanza pale Novemba 2010, hadi kufikia julai 08, 2015

Jitihada hizi ndizo zilizopelekea kutekelezwa kwa ilani ya chama cha Mapinduzi kwa kishindo, kwakuwa katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015, Halmashauri yetu imefanikiwa kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo na utoaji wa huduma kwa asilimia 90.

Katika Kipindi hiki Halmashauri imepiga hatua kubwa kwa kupanua wigo wa kimahusiano na taasisi nyingine hususani jeshi la Polisi, Magereza, LITA, TALIRI, TTC, CHUO CHA AFYA, taasisi za kifedha na asasi za kiraia. Ni kupitia mahusiano hayo mazuri yaliyopelekea Halmashauri kuendelea kunufaika. Kwa mfano waheshimiwa madiwani waliweza kujengewa uwezo na taasisi ya TARILI ambapo mafunzo waliyopewa, yamewafanya kuwa mstari wa mbele katika kuwa hamasisha

wakulima katika maeneo yao katika kufuata kanuni bora za kilimo na ufugaji. Vile vile halimashauri imeendelea kuwa katika hali ya utulivu wakati wote, na watoto wetu wameendelea kupata fursa za kujiendeleza kielimu.

Zipo shughuli nyingi zilizofanywa na baraza hili ikiwa ni pamoja na kupitisha rasimu ya kanuni ya za kudumu za uendeshaji wa Halmashauri za mwaka 2014, iliyoingiza vipengere vipya ili kuboresha nanma ya uendeshaji wa baraza katika ufanisi na tija. Moja wapo wa vipengere hivyo ni uwepo wa maswali ya papo kwa papo, kamati ya maadili kupandishwa hadhi na kuwa kamati ya kudumu na kuimbwa kwa wimbo wa taifa pamoja na kusoma dua kabla ya baraza.

Ni katika kipindi hiki ambapo Mpango kabambe wakupunguza umaskini kwa wananchi wetu umezinduliwa kupitia Progamu ya TASAF III. Programuu hii imezinduliwa katika Halmashauri yetu tarehe 10.04.2014 ambapo wananchi katika ngazi ya kaya maskini wanaendelea kunufaika na mpango huu utakaotekelezwa kwa miaka 10.

Maeneo mengi duniani masuala ya ardhi yameonekana kuwa na migogoro iliyoleta maafa. Halmashauri kupitia Idara ya Ardhi, imeendelea kuweka mipango madhubuti ya matumizi bora ya ardhi kwakushirikiana na wadau mbalimbali ambapo imeendelea kutoa elimu dhidi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Vile vile utaratibu wa uwazi katika ugawaji wa viwanja umezingatiwa ambapo hadi sasa kuna kamati ya ugawaji wa viwanja na wananchi hawatalazimika kulipa fedha ili kupimiwa viwanja badala yake Halmashauri ya wilaya itatafuta fedha kwaajili ya upimaji. Halmashauri imetumia kamati ya ugawaji wa viwanja kugawa viwanja na waliohitaji walipatiwa viwanja na orodha imewekwa wazi kupitia mbao za matangazo.

Pamoja na mwenendo mzuri katika Utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri yetu, kumekuwa na changamoto kama miradi kutekelezwa chini ya kiwango, wakandarasi kucheleweshewa malipo, Bajeti kutopata fedha zote hata hizo kidogo zinakuja kwa kuchelewa, nguvu za wananchi kutoungwa mkono na hivyo kuongeza miradi viporo na uanzishwaji holela wa miradi.

Halmashauri imeendelea kuchukua hatua mbali mbali za kukabiliana na chaangamoto hizi ikiwa ni pamoja na kukutana na watoa huduma na wakandarasi kupitia umoja wao na kupokea mawazo yao, kuendelea kuwasiliana na serikali ili ilete fedha na kuhamasisha wananchi ili wachangie miradi ya maendeleo.

Ushirikiano wetu mzuri umefanya , Halmashauri iendelee kuimarika siku hadi siku na kufanikiwa kuondoa hati yenye Mashaka mwaka **2010/2011** na kufanikiwa kupata Hati Safi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali **‘CAG’** tangu mwaka **2011/2012** hadi **2013/2014** (**miaka 3** mfululizo).

Kwa mara nyingine tena napenda kumshukuru Mungu kwa kutujalia kukutana hapa katika siku ya leo na pia napenda kwa dhati kuishukuru timu ya menejimenti na watumishi wote, na wananchi wa Halmashauri kwa kufanikisha mipango yote inayotukutanisha na kutuletea maendeleo.

Nashukuru pia ushirikiano ambao Halmashauri imeendelea kuupata kupitia ofisi ya Mkuu wa Wilaya ambayo kwa namna moja au nyingine tumeendelea kushirikiana katika kusimamia shughuli za uendeshaji wa Halmashauri

Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru viongozi wetu wa madhehebu ya dini, wamekuwa wakitulea kiroho kutukumbusha kutenda mema na haki katika kuwatumikia wananchi wetu. Zaidi wamekuwa wakituombea kwa Mungu na maombi yao yametufanya tusafiri salama katika katika kipindi chote cha oktoba 2010 hadi kufikia leo.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee wapiga kura wetu mliotupa dhamana ya kuwaongoza, tumewaongoza vyema katika kipindindi chote, hakika kazi mliyotutuma tumetekeleza, na tumeendelea kushirikiana nanyi katu hatukuwaangusha. Endapo mtatupa ridhaa kwa wakati mwingine na kama Mungu akipenda basi tutaendelea kutimiza haja ya mioyo yenu.

Ndugu zanguni, na wanasiasa wenzangu, wahenga walinena kuwa “mbio za sakafuni huishia ukingoni”, “tena kakuna marefu

yasiyokuwa na ncha". Maandiko pia yana tukumbusha "Kila jambo lina wakati wake"

Hata kama mioyo yetu ina dhamira ya dhati yakuendelea kuwatumikia wananchi wetu katika kuendeleza yale mema tuliyoyaanzisha, hatuna budi kurejea katika maeneo ya kata zetu ili tuweze kupata ridhaa ya kurudi kwa awamu nyingine ya kipindi cha mwaka 2015/2020.

Katika kipindi ambacho hatutakuwepo ni matumaini yangu kuwa tunawaacha katika hali ya utulivu na amani. Sasa muendelee kutekeleza majukumu yenu kwa kuzingatia kanuni na taratibu za uendeshaji wa Halmashauri ili malengo yaliyokusudiwa ya Halmashauri yaweze kufikiwa.

Nawatakia kila laheri katika utekelezaji wa majukumu yenu Tuendelee kuombeana.